



81 Angas Street, Adelaide  
South Australia 5000  
Simu: (08) 8206 8900  
Kuita bure: 1800 773 520  
Fax: (08) 8223 2218  
Mtandao: [www.sttars.org.au](http://www.sttars.org.au)



STTARS usaidia wakimbizi na wahamiaji waliopambana na uzoefu wa mateso ao waliokuwa wakitishika kufuatana na matukio ya mateso, unyanyasaji, vita, ao kifungo kinyume na sheria.

STTARS utoa ushauri kipekee ao kwa kundi, msaada na utetezi, tiba kwa kufinya na tiba nyingine za mambo za kiasili.

Kwa kupanga rufaa ao uteuzi, ita STTARS kwenye 8206 8900 kati ya saa tatu asubui na saa kumi na moja kiisha mchana, siku ya kwanza mpaka siku ya tano.

STTARS ni shirika lisilokuwa la kiserkali na pia kampuni tanzu lisilohusika na siasa wala dini. Tumekuwa tukitoa huduma kwa waathirika wa mateso na majeraha tangu mwaka wa 1991. Tupo wanamemba wa Jukwa la Huduma la Australia kwa Waathirika wa Mateso na kiwewe.

**Ita STTARS kama upo mkimbizi ao muhamiaji anayepambana na:**

Ugumu kwa kulala, kusitojisikia mwenyewe kimwili, ndoto za kutisha, wasiwasi na mashambulizi za hofu, huzuni mkubwa na kwa muda mrefu, hatia kubwa ao hasira ya muda mrefu, huzuni wa muda mrefu ao kumbukumbu ya kutisha, kupoteza kumbukumbu na kuhusu hali ya unyonge.

**Ao ujikuta mwenyewe:**

ukiepuka hali zinazokukumbusha hali mbaya iliopita, kujisikia upekee na kusitoaminia wengine, kusitoweza kuwa makini, kila mara kufikiria yaleyale, mara nyingi kupatwa na hisia bila sababu, kujisikia kuwa mbali na watu wanapokukaribia na kujiondosha kwenye marafiki na shughuli za kijamii.

**STTARS utoa Wakalimali.**

Ukihitaji mkalimali ahusiane nasi ita kwenye 131 450.

**STTARS utumika Kisiri.**

Hii uhimarisha ya kwamba hatutapana taarifa yako kwa mtu yeyote njee ya STTARS isipokuwa umekubaliana nayo

**Bure.**

Hii uimarisha ya kwamba haitakuwa na garama yeyote kifedha kwa kutumia huduma wetu.

**Jinsi ya kupata STTARS**

81 Angas Street, Adelaide  
South Australia 5000

**Simu:** (08) 8206 8900

**Kuita bure:** 1800 773 520

**Fax:** (08) 8223 2218

**Mtandao:** [www.sttars.org.au](http://www.sttars.org.au)

**Kusafiri na treni, basi ao tramu:**

Kutumia usafiri wa umma ni raisi zaidi kufika pa STTARS kwenye Angas Street na basi nyingi usimama pa Victoria Square. Zote namba 99c City Loop bus ilio ya bure, na Tramu ya Adelaide (ya bure kwenye City mjini) zasimama pa Victoria Square zikitokea kwenye Kituo Kikuu cha Reli cha Adelaide.